# MAENEO YA UWEKEZAJI MUHEZA.

## 1.0 HIFADHI YA ASILI YA AMANI NA UFUGAJI WA VIPEPEO

### 1.1 HIFADHI YA ASILI YA AMANI

Hifadhi ya Asili ya Amani ilitangazwa kisheria na Serikali ya Tanzania katika gazeti la serikali mwaka 1997, ikiwa na lengo la kuihifadhi bayoanuwai ya Milima ya Usamabara Mashariki. Safu ya Mashariki ya Milima ya Usambara imeorodheshwa kama kituo cha kimataifa cha bayoanuwai ya mimea na inajivunia kuwa ya pili kwa kuwa na aina nyingi za mimea katika bara la Afrika. Hifadhi hii ya viumbe hai yenye eneo la takribani hekta 83,600 inajumuisha misitu ya mvua na ardhi ya nyasi na miti ya uwanda wa chini. Ina sifa ya kuwa na mimea mingi iliyo katika hatari ya kutoweka (ikiwemo mimea mingi ya madawa) na ni makazi ya zaidi ya aina kumi na tatu za ndege wasiopatikana mahali pengine. Pia misitu hii mikuu hutoa maji kwa wakazi zaidi ya 300,000 katika mji wa Tanga, na wenyeji wa milimani wanategemea misitu hii kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kimaisha.

**Fursa na vivutio vilivyoko katika misitu ya Amani**

Mifumo ya ikolojia ya Usambara Mashariki iliharibiwa vibaya kuanzia miaka ya 1950 na kuendelea, kutokana na ukataji mkubwa wa miti uliokuwa ukifanywa na makampuni ya kigeni. Kiwanda cha mbao kilianzishwa Tanga kwa ajili ya usindikaji wa miti ya Usambara na kutengeneza mbao nyembamba na kupanua kazi zake miaka ya 1970 kwa ufadhili wa shirika la maendeleo la Ufini. Baada ya kuupunguza msitu kwa kiasi kikubwa kutokana na uwekezaji wao katika Mradi wa Msitu wa Eneo la Mkusanyiko wa Maji Mashariki mwa Usambara (EUCFP), miaka ya 1990, Ufini iligeuka na kuanza kulihifadhi eneo la mkusanyiko wa maji, viumbe hai walio hatarini kutoweka na kuendeleza huduma za mfumo wa ikolojia kwa ajili ya jamii za wenyeji.

Watu binafsi pia wananufaika na hifadhi hiyo kwa kuwekeza katika mahoteli yanayowapatia kipato. Wananchi pia wanaotembeza watalii katika hifadhi hiyo wananufaika na ajira ambapo huchukua asilimia 60 ya mapato ya kutembeza watalii (*Tour Guiding Fees*), asilimia 20 ikibaki hifadhini na asilimia 20 nyingine ikienda kwenye vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo. Vivutio vingi vya utalii vilivyohifadhiwa vizuri ni ikiwemo Misitu ya Asili na Wanyama mbalimbali kama vile Kima wa Bluu (*Blue Monkey*), Mbega Weupe na Weusi (*Black and White Collabus*), Nyoka, vinyonga pembe tatu (*Three Hornes Chamelleon*), vipepeo na ndege wa aina mbali mbali ambao

baadhi yao husafiri umbali mrefu kutoka barani ulaya kwa ajili ya kukimbia baridi kali na kuzaliana katika hifadhi hiyo.Vivutio vingine vilivyopo katika hifadhi hii ni Maporomoko ya Maji (*Water Falls*) ambayo ni Derema, Chemka, Ndola na Pacha. Pia kuna vivutio vya Vilele vya Vilima *(viewpoints)* kama Kiganga, Ngua, Makanya, Mbomole na Kilimahewa.

Mbali na vivutio hivyo, kivutio kingine ambacho ni cha kipekee katika hifadhi hiyo ni aina ya Ua linaloitwa "*Saintpaulia*" ambalo lina rangi ya Zambarau "*Violeth Color*", Ua hilo pia linatumika kama nembo ya hifadhi hiyo. Upekee wa Ua hilo ni kwamba likipandwa sehemu nyingine yeyote duniani hubadilika rangi yake ya asili, Tafiti mbalimbali zimefanywa ikiwemo kujaribiwa kupandwa nchini Ujerumani na kutoa majibu hayo hayo. Pamoja na vivutio hivyo kivutio kingine katika hifadhi hiyo ni mashine ya kusagia unga iliyokuwa ikitumia nishati ya nguvu ya kusukumwa na maji miaka 1986 katika kijiji cha Kisiwani na mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati hiyo hiyo iliyotumiwa na Wakoloni wa Kijerumani katika Kijiji cha Chemka.

Pia kuna Bustani ya Mimea ya Amani iliyoanzishwa mwaka 1902 chini ya utawala wa kikoloni na bado ni moja ya bustani kubwa kabisa za mimea Afrika. Hifadhi hii imeendelezwa kama kituo cha utalii, kikiwa na hoteli mbili na njia za kupita msituni, na pia kimekuwa kivutio kikubwa kwa watafiti wa ndani na nje. Tunawakaribisha wawekezaji katika sekta ya utalii kwenye milima ya Amani na watalii kwa ujumla.

**Maporomoko ya maji katika mto Ziggi**

Sehemu ya barabara zilizomo ndani ya Hifadhi ya misitu ya Amani



Sehemu ya barabara zilizomo ndani ya Hifadhi ya misitu ya Amani



**Watalii kutoka nchini Marekani wakifanya utalii katika misitu ya Amani**



**Kilimo cha uyoga; majiko ya nishati kidogo**

Katika sehemu ambazo vikundi vya wanawake vimekuwa vikikusanya mboga za majani katika maeneo makuu ya bayoanuwai ya hifadhi, mafunzo yametolewa ili kuendesha bustani nje ya maeneo ya bayoanuwai, ikiwa ni pamoja na kilimo cha uyoga. Kadhalika, mahali ambapo jamii za wenyeji zilitegemea zaidi kuni kutoka katika hifadhi, na wanawake wakiwa na kazi kubwa zaidi, majiko ya nishati kidogo yametolewa kwa vijiji vyote na jamii za maeneo ya karibu na Hifadhi ya Asili ya Amani.

**Kilimo cha Misitu na Urejeshaji wa Miti iliyokatwa**

Amani inajihusisha na shughuli za kilimo cha misitu katika maeneo ya mpaka wa hifadhi ili kuweka mfumo endelevu wa usimamizi wa mazao ya misitu na kupunguza utegemezi wa wenyeji kwa bayoanuwai ya hifadhi. Mipango ya vijiji ya usimamizi wa maliasili imeendelezwa ikizihusisha jamii za wenyeji na vijiji katika maamuzi ya matumizi ya rasilimali. Katika shughuli zote za kilimo cha misitu na urejeshaji wa misitu, spishi za miti zinachaguliwa kwa makubaliano kwa kushauriana na jamii za wenyeji. Shughuli hizi zimejikita katika kupanda spishi za kienyeji na kuzuia kusambaa kwa spishi za kigeni.

**Maporomoko ya maji yanayotokana na Hifadhi ya Bioanuai ya milima ya Amani wilayani Muheza**



## 1.1 MRADI WA UFUGAJI WA VIPEPEO AMANI

Wilaya ya Muheza katika msitu wa hifadhi wa Amani, kuna aina mbalimbali za vipepeo ambao kwa asili hawapatikani mahali pengine popote duniani. Njia nyingine mbadala ya kuendesha maisha kwa wakazi walioko katika milima ya Amani ni ufugaji wa vipepeo. Amani ina ushirikiano na shirika la madawa la ulaya ambalo hununua vipepeo wachanga, na kuwa chanzo kikubwa cha kipato kwa wakulima wenyeji.

Shughuli hizi za ufugaji wa vipepeo zimeanzishwa zikiwa na viwango mbalimbali vya mafanikio ya kupunguza athari za binadamu kwa mfumo wa ikolojia ya msitu, pasipo kuharibu bayoanuwai ya hifadhi

**Kibanda maalum kwa ajili ya ufugaji wa vipepeo katika kijiji cha Fanusi wilaya ya Muheza**







## 2. KILIMO CHA MACHUNGWA

**Utangulizi**

Mazao ya kibiashara yanayolimwa Muheza ni kama machungwa, chai, mazao ya viungo ( iliki, mdalasini na karafuu) miwa, nazi, katani, kokoa na korosho. Uzalishaji wa mazao ya kibiashara kwa mazao 9 makuu katika muda wa miaka 4 mfululizo ni tani 84,436.80 kwa mwaka 2010/2011, tani 100,657.50 kwa mwaka 2011/2012, tani 105,764 kwa mwaka 2012/2013, tani 112,419.56 kwa mwaka 2013/2014 na tani 1,655,699 kwa mwaka 2013/2014. Jedwali hapo chini laonesha

**Jedwali Na 2: Uzalishaji kwa tani kwa mwaka 2011/12 hadi 2014/15**

| **Mazao** | ***2010/11*** | ***1011/12*** | ***2012/13*** | **2013/14** | **2014/2015** |
|---|---:|---:|---:|---:|---:|
| Nazi | 21,992 | 18,359 | 22,959 | 3,119.96 | 3,983.4 |
| Mihogo | 49,796 | 66,920 | 53,183 | 71,590 | 45,570 |
| Machungwa | 59,872 | 79,930 | 80,430 | 101,849.60 | 93,086 |
| Korosho | 100 | 118 | 121 | 229.2 | 98 |
| Iliki | 718 | 578 | 756 | 165.7 | 161.2 |
| Mdalasini | 77 | 88.4 | 106 | 198.5 | 232 |
| Karafuu | 71 | 59.6 | 77 | 380.6 | 487 |
| Chai (Wakulima wakubwa) | 1,455 | 1,135 | 873 | 1,819 | 2,759 |
| Chai (Wakulima wadogo) | 96.8 | 97 | 92 | 136 | 134 |
| Katani | 55 | 292.5 | 350 | 477 | 1,550 |
| **Jumla Kuu** | **84,436.8** | **100,657.5** | **105,764** | **108,375.56** | **102,490.6** |

*CHANZO;* Ripoti ya kilimo ya wilaya (2015/2016)

## 2.1 UZALISHAJI WA MACHUNGWA MUHEZA.

Asili kuu ya spishi ya machungwa yanayolimwa Muheza ni kutoka Asia Mashariki na ilipelekwa na wafanyabishara wa kiarabu kwenda katika ukanda wa kimeditariani. Baada ya hapo spishi hii ikaletwa katika ukanda wa kitropikali na Wafanyabiashara wa kiarabu na Wareno. Inaaminika kwamba Wamisionari walileta chungwa kwa mara ya kwanza hapa Tanzania na walileta wilaya ya Muheza katika miaka ya 1900. Baada ya kugundua kuwa machungwa yanastawi katika hali ya hewa ya iliyopo, maeneo mengine ya kuendeleza zao hili yalitambuliwa na miche ilisambazwa na Wamisionari na wamiliki wa mashamba makubwa. Baada ya muda mfupi wakulima wadogo walianza kujishughulisha na kilimo cha machungwa kwa kusambaza mbegu na utaalamu. Mwanzoni mwa miaka ya 1970, Wizara ya Kilimo ilianza kutekeleza Mpango wa miaka mitano wa kuboresha uzalishaji wa matunda nchini Tanzania ikiwemo machungwa. Lengo kuu ilikuwa ni uanzishwaji wa vitalu vya wilaya kwa ajili ya kuzalisha miche ya machungwa, uanzishwaji wa vitalu vikuu. Wasambazaji wa miche walipewa miche ya milimau iliyoungwa na kuisambaza kwa wakulima bila malipo. Hata hivyo uendeshaji wa vitalu hivi haukuwa na msingi ya kibiashara na hivyo kutokuwa endelevu; kitalu cha mwisho kilifungwa miaka mitatu baada ya mradi huo kufikia ukomo mwaka 1977.

Katika wilaya ya Muheza machungwa huzalishwa kila mwaka. Kila baada ya miezi minne mchungwa hutoa maua na miezi miwili baadae machungwa hukomaa ambapo uzalishaji ni kwa misimu miwili kwa mwaka. Kipindi cha Septemba hadi Novemba ni msimu wa uzalishaji mdogo wakati kipindi cha mwezi desemba hadi aprili ni msimu wa uzalishaji mkubwa. Aina za machungwa yanayozalishwa wilaya Muheza ni pamoja na Valencia early and Valencia late (Msasa), Mediterranean sweet (Nairobi), Jaffa, Washington and Matombo sweet.

**Hali ya Uzalishaji wa machungwa**

**Ukubwa wa mashamba**

Katika wilaya ya Muheza, wakulima wa machungwa wamegawanyika katika sehemu kuu tatu kutoka na ukubwa wa mashamba ya machungwa. Wakulima wadogo (wenye hekta ½ hadi hekta 2), Wakulima wa Kati (wenye hekta 2 hadi 6) na wakulima wakubwa (wenye zaida ya hekta 6), jedwali hapo chini linaonesha.

**Jedwali Na 3. Classification of Farm Size**

| **Aina ya wakulima** | **Ukubwa wa mashamba yanayomilikiwa** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Wakulima wadogo | ½ hekta - 2 | 73 |
| Wakulima wa Kati | Hekta 2 - 6 | 23 |
| Wakulima wakubwa | Zaidi ya hekta 6 | 4 |

Ingawa kuna idadi kubwa ya wakulima wadogo wilayani, kwa sasa kuna maendeleo ya mashamba makubwa ya machungwa ya kati, ambapo inaonesha kuwa kiashiria cha mwelekeo mzuri katika maendeleo ya mashamba ya machungwa wilayani

**Uzalishaji**

Uzalishaji wa machungwa wilayani Muheza umeongezeka kutoka tani 79,930 mwaka 2010/11 kwa mwaka hadi tani  221,195 kwa mwaka mwaka 2014/2015.

**Uzalishaji wa machungwa kwa tani kwa hekari**




Uzalishaji wa machungwa kwa tani kwa hekari unabadilika badilika kutokana na kubalika kwa kiasi cha mvua kinachonyesha kutokana na hali ya hewa na magonjwa mbalimbali yanayoathiri machungwa.

**Jedwali Na 4: Uzalishaji wa machungwa kwa tani kwa mwaka**

| Years | 2011/2012 | 2012/2013 | 2013/2014 | 2014/2015 | 2015/2016 |
|---|---|---|---|---|---|
| Uzalishaji kwa tani | 79,930 | 80,430 | 101,849.60 | 93,086 | 221,195 |
| Hekta zilizolimwa | 8,043 | 8,069 | 11,063.70 | 11,635.8 | 12,288.60 |
| Wastani wa uzalishaji kwa tani kwa hekta | 9.94 | 9.97 | 9.21 | 8.0 | 18.00 |

**Changamoto za Uzalishaji wa machungwa**

Uzalishaji wa machungwa wilayani Muheza unakabiliwa na changamoto zifuatazo.

i. **Ukosefu wa fedha/mitaji**

Ukosefu wa fedha/mtaji kwa ajili ya kuendesha kilimo ni mojawapo ya vikwazo kwa wakulima wadogo wa machungwa wilayani Muheza. Wakulima wengi hushindwa kuuza mazao ya katika masoko ya mbali kama Arusha, Moshi, Dar es salaam na Nairobi kutokana na ukosefu wa fedha za kusafirisha mazao haya kwakuwa gharama za usafirishaji ni kubwa ukilinganisha na gharama zyingine za uzalishaji. Hii hupelekea wakulima kuuza mazao yao kwa bei ya shamba pengine kwa njia ya kuwekeza ambayo haimpi unafuu mkulima. Baadhi ya wakulima hushindwa kulihudumia shamba kwa kulima na kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao kwa sababu za kukosa fedha.

ii. **Ukosefu wa soko**

Ukosefu wa soko ni changamoto nyingine inayoathiri wakulima wa machungwa katika wilaya ya Muheza. Tafiti zinaonesha kuwa wakulima wengi huuza machungwa yakiwa juu ya mti bila ya kufikisha sokoni. Hii husababisha kukosekana kwa soko la uhakika la zao la machungwa. Wafanyabiashara hutumia madali kutafuta mazao shambani ni hii hupunguza kipato kwa mkulima kwa kuwa dalali huchukua nyongeza ya bei ya kila chungwa kwa mkulima.

**Picha ya mti wa mchungwa aina ya Valensia**



**Kitalu cha miche ya machungwa katika kata ya Mtindiro**

